

# UTAFITI WA VIASHIRIA NA MATOKEO YA UKIMWI TANZANIA (THIS) 2016 - 2017



Utafiti wa Viashiria na Matokeo ya UKIMWI nchini Tanzania ni utafiti wa kitaifa uliofanyika katika ngazi ya kaya kuanzia mwezi Oktoba, 2016 mpaka mwezi Agosti, 2017 ili kujuu hali ya maambukizi ya Virusi Vyta UKIMWI (VVU) kitaifa. Utafiti huu ulitoa huduma

za ushauri nasaha, upimaji wa VVU na utoaji wa majibu pia ulikusanya taarifa za kaya na taarifa binafsi za wanakaya, upatikanaji wa huduma na matibabu kwa watu wanaoishi na VVU. Utafiti huu uliopima maambukizi mapya ya VVU na kiasi cha VVU mwilini kwa watu wanaoishi na VVU ni wa kwanza kufanyika nchini. Matokeo ya utafiti huu yanatoa taarifa katika ngazi ya kitaifa na mikoa kwa ajili ya ufuatiliaji wa udhibiti wa VVU.

Utafiti wa THIS wa mwaka 2016-17 umeongozwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuitia Tume ya Kuthibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Zanzibar (ZAC), na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Afya, Zanzibar, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu, Zanzibar. Utafiti wa THIS umefadhiliwa na Serikali ya Marekani chini ya Mfuko wa Dharura wa Kupambana na UKIMWI (*President's Emergency Plan for AIDS Relief -PEPFAR*) na msaada wa kiufundi umetolewa na Kituo cha Kudhibiti Magonjwa ya Kuambukiza cha Marekani (*Center for Disease Control and Prevention -CDC*) na '*International Centre for AIDS Care and Treatment Programme (ICAP) at Columbia University*'.

Utafiti huu umefanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu, Zanzibar na ICAP kwa kushirikiana na wadau wengine wakiwemo Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii, Uhakiki, Ubora na Mafunzo (*National Health Laboratory - Quality Assurance and Training Center -NHL-QATC*), Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP), na Kitengo Shirikishi cha UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma (ZIHTLP) cha Zanzibar.

## MATOKEO MUHIMU

Viashiria vya VVU	Wanawake	95% CI	Wanaume	95% CI	Jumla	95% CI
<b>Maambukizi Mapya ya VVU</b>						
kwa mwaka (%)						
Miaka 15-49	0.34	0.18-0.50	0.14	0.02-0.26	0.24	0.14-0.35
Miaka 15-64	0.34	0.19-0.50	0.17	0.05-0.29	0.25	0.15-0.36
<b>Kiwango cha Maambukizi ya VVU-Tanzania (%)</b>						
Miaka 15-49	6.2	5.7-6.7	3.1	2.7-3.5	4.7	4.3-5.0
Miaka 15-64	6.5	6.0-7.0	3.5	3.1-3.9	5.0	4.7-5.4
Miaka 0-14	0.5	0.2-0.8	0.3	0.1-0.5	0.4	0.2-0.6
<b>Kiwango cha Maambukizi ya VVU- Tanzania Bara (%)</b>						
Miaka 15-49	6.4	5.8-6.9	3.1	2.7-3.6	4.8	4.4-5.1
Miaka 15-64	6.7	6.1-7.2	3.6	3.2-4.0	5.1	4.8-5.5
Miaka 0-14	0.5	0.2-0.8	0.3	0.1-0.5	0.4	0.2-0.6
<b>Kiwango cha Maambukizi ya VVU -Zanzibar (%)</b>						
Miaka 15-49	0.8	0.2-1.5	0.0	0.0-1.0	0.4	0.1-0.8
Miaka 15-64	0.8	0.2-1.5	0.0	0.0-0.8	0.4	0.1-0.8
Miaka 0-14	0.0	0.0-2.3	0.0	0.0-1.9	0.0	0.0-1.9

Viashiria vya VVU	Wanawake	95% CI	Wanaume	95% CI	Jumla	95% CI
<b>Kufubazwa kwa VVU Mwilini (%)</b>						
Miaka 15-64	57.5	54.0-61.01	41.2	35.7-46.7	52.0	48.6-55.4
Miaka 0-14	11.7	0.0-23.8	*	*	18.4	4.6-32.3

95% CI (kiwango cha uhakika) kinaonyesha kwamba makisio yatakuwa ndani ya kigezo sahihi kwa asilimia 95%. Kufubazwa kwa VVU mwilini ni wakati ambapo HIV RNA ni chini ya 1,000 kwenye milimita 1 ya plasma kwa watu wenye VVU, Vipimo vya Maambukizi mapya vinatokana na MDRI ya siku 130. \* inammaanisha < 0

\* Hakuna taarifa za Kufubazwa kwa VVU kwa watoto wa kiume wenye miaka 0-14 kwa sababu ya kutokuwa na sampuli ya kutosha ya kuweza kutoa makadirio katika umri huu

Maambukizi mapya ya VVU kwa mwaka kwa watu wenye umri wa miaka 15-64 nchini ni asilimia 0.25 (kwa wanawake ni asilimia 0.34 na wanaume ni asilimia 0.17). Hii ni sawa na kusema maambukizi mapya kwa watu wenye umri kati ya miaka 15-64 nchini Tanzania ni takribani watu 72,000 kwa mwaka.

Kiwango cha maambukizi ya VVU kwa watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 nchini ni asilimia 5.0 (kwa wanawake ni asilimia 6.5 na asilimia 3.5 kwa wanaume). Hii ni sawa na kusema kwa wastani watu milioni 1.4 wenye umri wa miaka 15 hadi 64 wanaishi na virusi vya UKIMWI nchini Tanzania.

Asilimia 52 ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 wanaishi na virusi vya UKIMWI nchini Tanzania, vipimo vinaonesha kuwa kiasi cha VVU mwilini kimefubazwa (kwa wanawake ni asilimia 57.5 na wanaume ni asilimia 41.2).

## KIWANGO CHA MAAMBUKIZI YA VVU KWA UMRI NA JINSI

Hali ya maambukizi ya VVU imefikia asilimia


12 kwa wanawake wenyewe umri wa miaka

45-49 ikilinganishwa na asilimia 8.4 ya  
wanaume wenyewe umri wa miaka 40-44.

Hali ya maambukizi ya VVU kwa watu  
wenye umri wa miaka 15-24 ni asilimia 1.4

(kwa wanawake wenyewe umri huu ni  
asilimia


2.1 na wanaume ni asilimia 0.6). Tofauti  
kubwa ya hali ya maambukizi ya VVU kati ya  
wanawake na wanaume imeonekana zaidi  
kwenye kundi la vijana, ambapo hali ya  
maambukizi ya VVU kwa wanawake wenyewe  
umri wa miaka 15-19, 20-24, 25-29, 30-34 na  
35-39 ni mara mbili (au zaidi) ikilinganishwa  
na wanaume wa kundi la umri huo.



## KIWANGO CHA MAAMBUKIZI YA VVU KWA WATU WAZIMA, KIMKOA

Kiwango cha maambukizi kwa watu wenyewe umri  
wa miaka 15 na zaidi kinatofautiana kimkoaa nchini

Tanzania kutoka asilimia 11.4 mkoa wa Njombe hadi  
chini ya asilimia moja kwa mkoa wa Lindi na  
Zanzibar.




\* Inamaanisha hakuna maambukizi (<1) au 'zero cases'

Mkoa	Kiango cha Maambukizi ya VVU	95% CI
Dodoma	5.0	2.6-7.5
Arusha	1.9	0.6-3.3
Kilimanjaro	2.6	1.7-3.4
Tanga	5.0	3.2-6.7
Morogoro	4.2	3.0-5.3
Pwani	5.5	4.3-6.8
Dar es Salaam	4.7	3.7-5.6
Lindi	0.3	0.0-0.8
MtWARA	2.0	0.0-4.2
Ruvuma	5.6	4.4-6.7
Iringa	11.3	9.0-13.6
Mbeya	9.3	7.4-11.2
Singida	3.6	0.6-6.5
Tabora	5.1	4.2-6.0
Rukwa	4.4	3.4-5.4
Kigoma	2.9	1.6-4.3
Shinyanga	5.9	5.3-6.5
Kagera	6.5	4.1-8.8
Mwanza	7.2	4.9-9.4
Mara	3.6	2.5-4.7
Manyara	2.3	1.1-3.5
Njombe	11.4	7.5-15.3
Katavi	5.9	4.3-7.5
Simiyu	3.9	2.3-5.6
Geita	5.0	3.0-7.0
Songwe	5.8	3.5-8.1
Kaskazini Unguja	0.6	0.0-1.8
Kusini Unguja	0.0	0.0-0.0
Mjini Magharibi	0.6	0.1-11.1
Kaskazini Pemba	0.0	0.0-0.0
Kusini Pemba	0.3	0.0-0.9

## KUFUBAZWA KWA VVU MWILINI KWA WATU WANAOISHI NA VVU, KWA UMRI NA JINSI


Kiasi cha VVU mwilini kwa watu wenye maambukizi ya VVU nchini Tanzania kimefubazwa kwa kiasi kikubwa kwa watu wazima, ambapo asilimia 64.4 ni kwa wanawake wenye umri wa miaka 55-64 na asilimia 61.5 ya wanaume wenye umri huo.

Kuna tofauti kubwa ya kijinsia ya kufubazwa kwa VVU mwilini katika makundi ya umri ambapo asilimia 47.1 na 50.5 ya wanawake wenye umri wa miaka 15-24 na miaka 25-34 virusi vyao vimefubazwa na kwa wanaume wa makundi hayo ya umri ni asilimia 22.2 na 25.7 virusi vyao vimefubazwa.



## KUFUBAZWA KWA VVU MWILINI KWA WATU WANAOISHI NA VVU, KIMKOA

Kati ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi wenye maambukiziya VVU, kufubazwa kwa VVU mwilini kunatofautiana kimkoa nchini Tanzania, kutoka asilimia 66 mkoa wa Kagera na asilimia 67‡ mkoa wa Kilimanjaro hadi asilimia 40 mkoa wa Shinyanga na asilimia 29‡ mkoa wa Arusha.



‡ Inaonesha, namba ya chini ya mstari (denominator) ni chini ya 50

† Inaonesha, namba ya chini ya mstari (denominator) ni chini ya 25

\* inaonyesha hakuna maambukizi


Mkoa	Kufubazwa kwa VVU	95% CI
Dodoma	60.6‡	35.7-85.5
Arusha	29.1†	4.1-54.0
Kilimanjaro	66.8†	46.8-86.8
Tanga	47.2‡	37.4-57.0
Morogoro	45.3‡	23.9-66.6
Pwani	63.5	53.9-73.0
Dar es Salaam	44.7	36.7-52.7
Lindi	100.0%†	100.0-100.0
Mtwara	53.3†	43.8-62.8
Ruvuma	56.7	45.8-67.5
Iringa	56.6	49.0-64.2
Mbeya	57.4	47.6-67.1
Singida	40.4%†	0.0-83.1
Tabora	41.2	30.6-51.7
Rukwa	42.9	31.5-54.2
Kigoma	58.4%†	36.1-80.6
Shinyanga	40.1	30.1-50.1
Kagera	66.0	53.4-78.5
Mwanza	49.6	39.2-60.0
Mara	63.4%‡	51.4-75.4
Manyara	36.6%†	9.7-63.5
Njombe	60.5	46.6-74.4
Katavi	47.3	38.3-56.4
Simiyu	54.3%‡	28.2-80.4
Geita	32.4%‡	21.3-43.6
Songwe	64.6	52.6-76.7
Kaskazini Unguja	44.5%*	42.3-46.7
Mjini Magharibi	21.0%*	0.0-65.9
Kaskazini Pemba	*	*
Kusini Pemba	0†	0.0-0.0

### 90-90-90: Lengo la Matarajio Makubwa la Kumaliza Janga la UKIMWI

Hadi kufikia mwaka 2020, asilimia 90 ya watu wanaoishi na VVU wawe wamejua hali yao ya maambukizi; asilimia 90 ya waliopimwa VVU na kugundulika kuwa wana maambukizi ya VVU wapatiwe dawa za kufubaza makali ya VVU; na asilimia 90 ya watu wanaotumia dawa, VVU viwe vimefubazwa.

#### Waliopimwa na Kugundulika na Maambukuzi ya VVU

Nchini Tanzania, asilimia 60.6 ya watu wanaoishi na VVU wenyе umri wa miaka 15-64 ambaо wanajua hali zao za maambukizi ya VVU (kwa wanawake ni asilimia 64.9 na wanaume ni asilimia 52.2).



#### Wanaotumia Dawa

Kati ya watu wanaoishi na VVU wenye umri wa miaka 15-64 ambaо wanajua hali zao za maambukizi ya VVU, asilimia 93.6 walitoa taarifa kwamba wanatumia dawa za kufubaza VVU (kwa wanawake ni asilimia 95.3 na wanaume ni asilimia 89.6).

#### Kufubazwa kwa VVU

Kati ya watu wanaoishi na VVU wenye umri wa miaka 15-64 ambaо wametoa taarifa kuwa wanatumia dawa za kufubaza VVU, asilimia 87.0 ya watu hao inaonesha kiasi cha VVU kimefubazwa (kwa wanawake ni asilimia 88.0 na wanaume ni asilimia 83.2).

### KIWANGO CHA MAAMBUKIZI YA HOMA YA INI B, KWA JINSI, UMRI NA HALI YA MAAMBUKIZI YA VVU

Utafiti wa THIS umepima pia kiwango cha maambukizi ya Homa ya Ini (Hepatitis) kwa sampuli ya watu wachache ili kupata makadirio ya kiwango cha maambukizi suga na ya kawaida ya Homa ya ini aina ya B. Kati ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi, kiwango cha mambukizi ya homa ya ini aina ya B hakina tofauti sana kwa watu wenye maambukizi ya VVU na ambao hawana maambukizi ya VVU. Japokuwa makadirio ya watu wenye VVU (5.2%) yapo juu ukilinganisha na watu wasiokuwa na maambukizi ya VVU (3.4%), Makadirio haya kitakwimu hayana tofauti. Makadirio ya kitaifa ya kiwango cha maambukizi ya kawaida au sugu ya homa ya ini aina B ni ya kwanza kutolewa nchini Tanzania na yatatumika kama msingi wa kuendeleza mwitikio wa udhibiti wa Homa ya Ini.

Hali ya VVU na Umri	Wanawake		Wanaume		Jumla	
	Kiwango cha Maambukizi ya Homa ya Ini B	95% CI	Kiwango cha Maambukizi ya Homa ya Ini B	95% CI	Kiwango cha Maambukizi ya Homa ya Ini B	95% CI
<b>Wario na VVU</b>						
Miaka 15-49	0**	0.0-10.9	*	*	4.3	0.0-11.3
Miaka 15+	0**	0.0 -7.1	*	*	5.2	1.8-8.6
<b>Wasio na VVU</b>						
Miaka 15-49	3.9	1.7-6.1	4.0	1.1-7.0	4.0	2.2-5.8
Miaka 15+	3.5	1.7-5.3	3.4	0.9-5.8	3.4	1.9-4.9
<b>Jumla</b>						
Miaka 15-49	3.7	1.6-5.8	4.3	1.4-7.2	4.0	2.3-5.8
Miaka 15+	3.3	1.6-5.0	3.8	1.4-6.2	3.5	2.1-5.0

95% CI (kiwango cha uhakika) kinaonyesha kwamba makisio yatakuwa ndani ya kigezo sahihi kwa asilimia 95%

\* Matokeo hayajatolewa kwa kuwa idadi ya "denominator" ni chini ya watu 25

\*\* Tahadhari, namba ya chini ya mstari (denominator) ya 25-49 cases

Upimaji wa vimelea kutambilisha maambukizi ya homa ya ini B unaonyesha kama kuna maambuzi mapya au ya zamani ya homa ya ini B umefanyika katika sampuli ndogo wakilishi ya watu 1,052 wenye umri wa miaka 15-49, na watu 1,310 wenye umri wa miaka 15 na zaidi.

- Inakadiriwa kuwa asilimia 60.6% ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi wanajua hali zao za maambukizi ya VVU ambapo ni chilni ya malengo ya UNAIDS ambayo ni asilimia 90. Inahitajika nguvu na programu za upimaji kwa watu wanaoishi na VVU (1<sup>st</sup> 90)
- Kuna tofauti ya ukubwa wa tatizo la VVU kimkoa na kijinsia ambalo ninatakiwa lipewe kipaumbele kwenye malengo ya kuzuia maambukizi ya VVU na matibabu.
- Wanawake wana kiwango kikubwa cha maambukizi mapya ya VVU ukilinganisha na wanaume. Kwa mwaka, kuna wanawake wawili kwa kila ambukizi jipya la wanaume.
- Wanaume wana kiwango kidogo cha uelewa wa hali zao za maambukizi kuliko wanawake. Wanaume pia wana kiwango kidogo cha matibabu (90 ya pili) na kufubazwa kwa VVU (90 ya tatu) ukilinganisha na wanawake. Kuzuia maambukizi ya VVU kwa wanawake na vipimo vya haraka vya VVU ukijumlisha na kuunganisha wenyne VVU kwenye matibabu pamoja kufubazwa kwa VVU mionganoni mwa wanaume ni muhimu katika kuzuia maambukizi.
- Kiwango kidogo cha kufubazwa kwa VVU kwa watoto kinaonesha uhitaji wa jitihada zaidi katika upimaji na matibabu ya watoto wenyne VVU

## MWITIKIO NA NJIA ZA UPIMAJI WA VVU

Kati ya kaya 15,504 zilizostahili kushiriki katika utafiti wa Viashiria na Matokeo ya UKIMWI, kaya 14,811 (asilimia 95) zilishiriki na kukamilisha mahojiano ya kaya. Kati ya wanawake 19,852 na wanaume 16,235 walostahili kuhojiwa wenyne umri wa miaka 15 na zaidi, asilimia 90 ya wanawake na asilimia 85 ya wanaume walihojiwa na kupimwa VVU. Kati ya watoto 10,452 wenyne umri wa miaka 0 – 14 , asilimia 92 walipimwa VVU. Sampuli wakilishi ya watu 1,310 wenyne umri wa miaka 15 na zaidi walipimwa vimelea vya kutambulisha homa ya ini aina ya B. ili kujuu kama kuna maambukizi mapya au ya zamani ya homa ya ini B umefanyika katika sampuli ndogo wakilishi ya watu 1,052 wenyne umri wa miaka 15-49, na watu 1,310 wenyne umri wa miaka 15 na zaidi.

Upimaji wa kiwango cha maambukizi ya VVU ulifanyika kwenye kila kaya iliyoshiriki katika utafiti kwa kutumia kipimo cha VVU kulingana na miongozo ya upimaji ya Tanzania. Kipimo kingine cha damu kilitumika katika maabara ili kuhakiki majibu ya watu walioonekana kuwa na VVU. Kipimo cha kupima maambukizi mapya na kiasi cha virusi mwilini (*HIV 1 Limiting Antigen (Lag) avidity plus viral load and ARV results*) kilitumika kutofautisha maambukizi mapya na ya zamani na kipimo kingine kiitwacho ‘CDC Incidence calculator’ kinachotambuliwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kilitumika. Njia ya kitakwimu ilitumika katika makadirio ya sampuli ili kuwalilisha kundi kubwa la watu katika utafiti huu.

**Utafiti wa Viashiria na Matokeo ya UKIMWI ambao ni  
sehemu ya Mradi wa Kutathmini Matokeo ya UKIMWI  
katika Jamii (PHIA) umefanyika kwenye nchi zaidi ya moja  
kwa kufadhiliwa na PEPFAR kwa ajili ya kutambua hali ya  
maambukizi ya VVU. Matokeo ya utafiti huu yanapima  
uali ya maambukizi ya VVU kitaifa na kimkoa pamoja na  
viashiria vinavyohusiana na VVU, ikijumuisha maendeleo  
ya malengo ya 90-90-90 na pia utatoa miongozo katika  
sera na ufadhili. Shirika la Kimataifa lisilo la Kiserikali la  
ICAP lililopo Chuo kikuucha Columbia linafanya mradi wa  
tafiti za VVU kwa ushirikiano na CDC na wadau wengine.**

Angalia [phia.icap.columbia.edu](http://phia.icap.columbia.edu) kwa maelezo ya ziada.



Alama ya "CDC" inamilikiwa na Idara ya Afya na Huduma za watu (HHS) ya Serikali ya Marekani kwa ruhusa. Utumiaji wa alama hii sio wa HHS au CDC kwa aina yoyote ya machapisho, au huduma

Utafiti huu umefadhiliwa na Serikali ya Marekani chini ya Mfuko wa Rais wa Dharura wa Kupambana wa UKIMWI (PEPFAR)" kwa kuititia CDC chini ya makubaliano namba U2GGH001226. Matokeo na hitimisho la chapisho hili ni ya waandishi wa chapisho (Authors) na sio lazima yahusianishwe na mashirika yaliyotoa fedha. Matokeo haya yachukuliwe kuwa ni ya awali na yanawenza kubadilika.